

T A N G A Z O



Mkuu wa wilaya ya Arusha **Mhe. Gabriel Fabian Daqarro** anawatangazia wananchi wote wa Jiji la Arusha kuwa, kesho Jumanne Tarehe **18.09.2018** tutaupokea Mwenge wa Uhuru katika jiji letu. Mapokezi ya Mwenge yataanza **1:00** Asubuhi eneo la **Chekereni** na utapita katika kata za **Moivaro, Oloirien, Moshono, Them, Daraja Mbili** na **Kati**. Mkesha utafanyika katika stendi ya hiace **Kilombero**.

Katika eneo la mkesha kutakuwa na burudani mbalimbali pamoja na huduma muhimu kama uzazi wa mpango, malaria, elimu ya mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI Pamoja na upimaji, kuchangia damu salama, mapambano dhidi ya dawa za kulevya ikiwa pamoja na elimu ya namna ya kupata mikopo isiyokuwa na riba kupitia 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri na maonyesho ya shughuli mbalimbali za wajasiriamali. Hakuna kiingilio ni bure kabisa.

Kauli mbiu ya mwaka huu “**Elimu ni ufunguo wa maisha, wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa**”

Wananchi jitokezeni kwa wingi kuupokea mwenge wetu.

Imetolewa na;

Mhe. Gabriel Fabian Daqarro

Mkuu wa Wilaya ya Arusha Mjini